


MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU WA VULI OKTOBA – DISEMBA, 2024



Kielelezo 1: Mwelekeo wa mvua za Oktoba hadi Disemba, 2024.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba – Disemba, 2024

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba - Disemba 2024, ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Utabiri huu ni mahsusii kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini, Ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma). Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

a) Mvua za Vuli, 2024

- i. Mvua zinatarajiwa kuwa za Chini ya Wastani hadi Wastani katika maeneo mengi na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.
- ii. Mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba, 2024 katika ukanda wa Ziwa Victoria na kusambaa katika maeneo mengine katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2024. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.
- iii. Mvua za Vuli zinatarajiwa kuongezeka kidogo mwezi Disemba, 2024.
- iv. Vipindi vya joto kali kuliko kawaida vinatarajiwa katika msimu wa Vuli.
- v. Uwepo wa La-Niña hafifu unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika mvua za msimu wa Vuli, 2024.

b) Athari zinazotarajiwa

- i. Upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi na hivyo kuathiri shughuli za kilimo.
- ii. Kina cha maji katika mito na mabwawa vinatarajiwa kupungua.
- iii. Kujitokeza kwa magonjwa ya mlipuko, kutokana na upungufu wa maji safi na salama.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Komyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

1. MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2024

Msimu wa mvua za Vuli ni mahususi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa katika kipindi chote cha msimu (kama inavyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), kwa ujumla mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hata hivyo, maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria yanatarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba, 2024 katika maeneo ya magharibi ya kanda ya Ziwa Victoria na kusambaa katika maeneo mengine katika mwezi Oktoba, 2024. Mvua zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024. Msimu unatarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo hususan mwezi Disemba, 2024.

Mbali na mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinazotarajiwa, vipindi vya joto kali kuliko kawaida vinatarajiwa katika msimu wa Vuli. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

i. Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo):

Mvua za Vuli zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi chini ya Wastani katika maeneo mengi ya Kanda ya Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba, 2024 katika mikoa ya Kagera, Geita na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na kutawanyika maeneo mengine katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2024. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Disemba, 2024.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz


(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

ii. Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):

Mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Oktoba, 2024 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.

iii. Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):

Mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Oktoba, 2024 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.



Angalizo 1: Ingawa upungufu wa mvua unatarajiwa katika maeneo mengi, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
 Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
 Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
 S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
 Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Angalizo 2: Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na utabiri wa kila mwezi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika msimu wa mvua wa Vuli, 2024 Joto la bahari la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kati la kitropiki la bahari ya Pasifiki, hali inayoashiria uwepo wa La-Niña. Vile vile, joto la bahari la Juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati ongezeko zaidi la joto juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kupunguza kasi ya msukumo wa unyevu nyevu kutoka Bahari ya Hindi kuelekea nchini hasa katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

Kwa upande mwingine, joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola). Kwa ujumla hali hii ya joto la bahari inatarajiwa kudhoofisha mifumo inayosababisha mvua nchini.

3. ATHARI NA USHAURI

Athari za kisekta na ushauri vimeandaliwa na TMA kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 19 Agosti, 2024. Wadau wa sekta za kiuchumi na kijamii wanashauriwa kupanga na kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia taarifa mahususi za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka.

a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Kipindi cha msimu wa mvua za Vuli, upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayopata mvua za Vuli hususan maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani ya kaskazini. Hali hii inatarajiwa kuathiri ukuaji wa mazao. Aidha, wadudu na magonjwa ya mazao yanatarajiwa kuongezeka katika msimu hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao. Vilevile, upatikanaji wa mazao ya misitu kama vile asali unatarajiwa kuathirika kutokana na uhaba wa maji na maua.

Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu na teknolojia za kilimo himilivu za kuhifadhi maji na unyevunyevu wa udongo. Aidha, wanashauriwa kuandaa mashamba kwa wakati, kupanda mbegu na mazao yanayoweza kukomaa kwa muda mfupi na yanayostahimili

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

ukame. Pia, wakulima wanashauriwa kupanda mazao tofauti tofauti yanayostahimili ukame ili kupunguza madhara yatakayoweza kujitokeza endapo zao moja litaathirika. Halikadhalika, mamlaka husika zinashauriwa kutoa elimu na uelewa kwa wakulima juu ya njia bora na namna ya kutumia kiwango kidogo cha mvua kinachotarajiwa pamoja na matumizi mazuri ya akiba ya chakula kilichopo. Wakulima pia wanahimizwa kupata ushauri kutoka kwa maafisa ugani kuhusu namna bora ya kuendesha shughuli za kilimo.

b) Mifugo na Uvuvi

Mvua chache zinazotarajiwa katika msimu zinaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na chakula kwa ajili ya samaki. Hali hii inatarajiwa kuathiri uzalishaji wa mifugo, mazao ya mifugo na samaki. Katika msimu huu, magonjwa kwa mifugo yanayoenezwa na kupe pamoja na wadudu warukao yanatarajiwa kupungua. Halikadhalika, kutokana na upungufu wa malisho na maji kuna uwezekano wa migogoro kujitokeza baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Vile vile, uzalishaji wa zao la mwani unaweza kuathirika kutokana na vipindi virefu vya ukavu na joto vinavyotarajiwa. Jamii inashauriwa kuweka mpango mzuri wa matumizi na uhifadhi wa maji na malisho. Aidha, wafugaji na wavuvi wanashauriwa watumie taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani.

c) Utalii na Wanyamapori

Mvua chache zinazotarajiwa zinaweza kupelekea uwepo wa upungufu wa chakula, na hivyo kusababisha migogoro kati ya jamii na wanyamapori kutokana na upungufu wa rasilimali. Kwa kuongezea, baadhi ya magonjwa ya wanyamapori yanayotokana na upungufu wa mvua yanaweza kutokea na hivyo kusambaa kwa magonjwa hayo kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa binadamu, kutokana na mwingiliano baina yao. Mamlaka husika zinashauriwa kuelimisha jamii kuchukua tahadhari kuhusiana na athari zinazoweza kujitokeza. Kwa upande mwingine, jamii iliyopo katika mazingira hatarishi inashauriwa kutoa taarifa ya uvamizi wa wanyamapori katika maeneo yao.

d) Usafiri na Usafirishaji

Sekta ya usafiri na usafirishaji hususan usafiri wa ardhini inaweza kunufaika kutokana na vipindi vya ukavu vinatarajiwa. Hata hivyo, inashauriwa kuwa kwa kipindi husika mipango ya uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji ifanyike kwa kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa uliohuishwa katika eneo husika.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

e) Nishati, Maji na Madini

Kupungua kwa kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kunatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani. Hali hii inaweza kupunguza upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali. Uzalishaji wa madini (hususan dhahabu kwa wachimbaji wadogo) na nishati ya umeme utokanao na maji unaweza kuathirika (unaweza kupungua). Katika sekta ya maji, watumiaji wanaweza kuathirika (kijamii, kiuchumi, na mazingira) na kupelekea migogoro kati ya watumiaji wakubwa na wadogo. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya maji, umeme, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi unatarajiwa kuendelea vizuri. Aidha, wadau wanasisitizwa kuzingatia mgawanyo wa maji na matumizi endelevu ya maji katika shughuli za kuchakata madini, uzalishaji wa umeme, matumizi viwandani na majumbani. Vile vile, mamlaka husika zinashauriwa kuwa na mipango madhubuti ya matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati.

f) Mamlaka za Miji

Kwa kuzingatia mvua za chini ya wastani zinazotarajiwa katika msimu wa Vuli, mamlaka za miji zinashauriwa kuongeza uelewa kwa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT) na madiwani ili kuendeleza mipango na bajeti kwa ajili ya maandalizi ya msimu katika sekta zinazotarajiwa kuathirika. Mamlaka za miji zinashauriwa kuhakikisha kuwa wadau wanaotoa huduma wanaratibiwa na kutoa taarifa za tahadhari za mapema zinazoshughulikia sekta mbalimbali. Kwa upande mwingine, mamlaka zinahimizwa kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha mifumo ya usambazaji wa maji safi na taka. Licha ya upungufu wa mvua kwa jumla, vipindi vifupi vya mvua kubwa vinatarajiwa, na hivyo kuhitaji maandalizi. Mamlaka za miji zinashauriwa kuhakikisha njia zote zinapitika vizuri kwa wakati wote na miundombinu iboreshwe ili kupunguza maji kujaa katika mifereji na mitaa.

g) Sekta ya Afya

Hali ya upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama inaweza kujitokeza na kusababisha magojwa ya mlipuko katika maeneo husika kama vile vikope, magonjwa ya ngozi, kipindupindu na homa ya matumbo; changamoto za kupumua na magonjwa yanayohusiana na joto kali. Mamlaka husika zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari hasi, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kutibu maji kabla ya kunywa, kusafisha matunda, kunywa maji safi, salama na ya kutosha ili kuepuka upungufu wa maji mwilini sambamba na kuzingatia usafi wa mwili na mazingira. Pamoja na hayo, mamlaka husika zinasisitizwa kutoa elimu ya afya kwa jamii ikiwemo kuzingatia usafi binafsi, matumizi ya maji safi na salama pamoja na usafi wa mazingira yanayowazunguka.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Komyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

h) Sekta Binafsi

Shughuli za kibiashara zinazohusisha hali ya hewa zinaweza kuathirika kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kutokana na matumizi makubwa ya nishati katika uhifadhi wa mazao tete na bidhaa. Mvua za Chini ya Wastani zinaweza kusababisha kuathirika kwa ubora wa miti ya nguzo na mbao. Wadau wa Sekta Binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalam mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Hatua za kupunguza matawi ya miti ya nguzo na mbao zitekelezwe mara kwa mara. Taasisi za Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

i) Menejimenti za Maafa

Upungufu wa mvua unaotarajiwa katika msimu huu unaweza kuleta madhara ya upatikanaji wa chakula, malisho ya mifugo na maji. Mamlaka husika zinashauriwa kushirikiana na kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula, malisho ya mifugo, maji na kutoa miongozo ya namna ya kukabiliana na maafa ili kuzuia na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Hivyo, mamlaka husika na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji zinashauriwa kushirikiana na kuchukua hatua za kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na maafa ikiwemo kutoa elimu na miongozo itakayohamasisha kilimo cha mazao yanayostahimili ukame, uhifadhi wa chakula, maji na malisho ya mifugo.

j) Vyombo vya Habari

Waandishi wa Habari wanashauriwa kufuatilia na kupata taarifa sahihi za utabiri na tahadhari ya Hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kuzisambaza kwa wakati ili kuelimisha umma na kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

Wanahabari wanashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa wataalam ili kuandaa na kusambaza makala na ripoti za kisekta kwa lugha rahisi kwa lengo la kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu matumizi ya utabiri katika kukabiliana na athari ya hali ya hewa ikiwa ni pamoja na upungufu wa mvua.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wote wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, mamlaka za wanyamapori, wasafirishaji, mamlaka za maji na afya kuendelea kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalam katika sekta husika.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

Imetolewa: 22 Agosti, 2024

Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)